

*Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (katikati waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na Sehemu ya Wawekezaji waliohudhuria kikao kilichoandaliwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) jijini Dodoma Mei 29, 2021.*

# Wawekezaji waiomba serikali kudhibiti uvamizi ranchi za taifa

NA MBARAKA KAMBONA,

WAWEKEZAJI wa muda mrefu katika Vitalu vya Ranchi za Taifa wameiomba Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti uvamizi unaofanywa na baadhi ya Wananchi katika maeneo hayo kwani vitendo hivyo vimekuwa kikwazo kikubwa katika kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini.

Wawekezaji walisema hayo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alipokutana nao katika kikao kilichoandaliwa na Kampuni za Ranchi za Taifa (NARCO) kilichofanyika jijini Dodoma Mei 29, 2021.

Wakieleza changamoto wanazozipata katika uwekezaji wao walisema kuwa pamoja na mambo mengine, suala la Wananchi kuvamia maeneo yao waliyowekeza linakwamisha kufanya shughuli zao za kuendeleza ufugaji wa kisasa.

Mwenyekiti wa Wawekezaji hao, Jackson Mwasonga alisema kuwa wavamizi wanakwamisha shughuli zao na kuna wakati wanalazimika kutoa hela kwa wavamizi hao ili waweze kuchunga mifugo yao katika maeneo wanayomiliki kihalali.

"Waziri inafika wakati tunatoa hela ili tuweze kuchunga na kunusuru mifugo yetu,uvamizi unatishia maisha yetu na mali zetu, tunaomba mtangaze wavamizi waondoke ili tuweze kufanya ufugaji unaohitajika kwa amani," alisema Mwasonga

Projestus Gamasho, Mwekezaji katika Ranchi ya Kitengule, Mkoani Kagera alisema ranchi hiyo kwa sasa imevamiwa na tembo zaidi ya Mia Sita (600) na wameharibu miundombinu yote huku akiomba Serikali kutoa msaada wa haraka kuwaondoa tembo hao.

Mwekezaj wa Ranchi ya Uvinza, Kigoma, Benard Katamba alisema wavamizi katika Ranchi hiyo sio tu wamechukua maeneo yao, wanaiba mifugo yao kila wakati jambo ambalo linawakatisha tamaa ya kuendelea na ufugaji.

Sisi Wawekezaji wa Ranchi ya Uvinza tumevamiwa haswa, mpaka sasa nimeshaibiwa ng'ombe 25 na mbuzi 150 na sina matumaini yoyote ya kuwapata, kwa kweli tunaomba msaada wa Serikali," alisema Katamba

Kufuatia hali hiyo, Mwekezaji katika Ranchi ya Misenyi, Mkoani Kagera, Nestory Lugakingira akitoa ushauri kwa Serikali alisema kuwa ili waweze kuishi kwa amani Serikali ione uwezekano katika yale maeneo yaliyovamiwa yagawiwe kwa wavamizi hao na sehemu itakayobaki waitumie kuendeleza mifugo yao na kuepuka migogoro na wananchi hao.

Akitoa ufafanuzi wa hoja za Wawekezaji hao, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema kuwa Serikali ipo pamoja na Wawekezaji hao na itachukua hatua kali kwa wale wote wanaovamia maeneo ya ranchi kinyume na Sheria.

# CCM Morogoro wampongeza Rais Samia kwa kubeba chama

NA MWANDISHI WETU

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Morogoro, Dorothy Mwamsiku,amempongeza Rais wa Tanzania ambaye pia Mwenyekiti wa Chama hicho Taifa,Samia Suluhu Hassan kwa kukikubeba Chama chao kuwalea na kuwapa heshima katika kila nyanja ndani na nje ya nchi.

Pia amezitaka kata 14 za manispaa ya Marogoro kuhakikisha zinaweka mipango ya uwanzishwaji wa miradi ndani ya kata na kuhakikisha wanajenga majengo ya Kupendeza ya Ofisi zao za Chama kwani ndio nembo ya Chama chao.

Akizungumza hayo jana wakati wa kuanza ziara yake ya kutembelea majimbo mbalimbali katika mkoa huo kwa lengo la kushukuru kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Mkoa huo,Mwamsiku alisema kutokana na kuongozwa na Rais mwanamke,ni vema wanawake wasijute kuzaliwa wanawake kwani wanaona kazi zilizofanywa na mwanamke kiongozi huyo ni jambo la kujivunia.

Alisema kwa sasa wanawake wanaweza,kwani yeye ni Mwenyekiti wa Kwanza kuongoza Chama hicho ndani ya Chama cha CCM ndani ya mkoa huo,hivyo ni wakati sahihi wa wanawake kujivunia.

" Chama chetu mkoa wa Morogoro kinampongeza kwa dhati Rais Samia kuchaguliwa kwake kwa kishindo kwa asilimia 100 kuwa Mwenyekiti wa Chama Taifa,hivyo tunahaidi kuendelea kumpa ushirikiano dhabiti kuhakikisha anaendelea kutuongoza vema,"alisema na kuongeza

"Pia nawapongeza wajumbe wa Halmshauri kuu ya Taifa wa Chama chetu katika kuchaguliwa kwao na kuongoza jahazi la wanaccm Taifa," alisema Mwamsiku

Alisema Uongozi ni Utumishi alipoamua kwenda kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya uwenyekiti ndani ya Chama chao mkoa wa Morogoro aliamua kuwatumikia wanachama wa Chama hicho na wale ambao sio wanachama wa Chama hicho akiwa Mtumishi wao.

Mwamsiku alisema hana kisasi wala malipizi kwani uchaguzi umeisha sasa kazi inaendelea ya kujenga Chama hivyo amehaidi atawatendea haki watu wote kwa kufuata kanuni,katiba na Muongozo wa Chama chao na kuhaidi kufanya kazi nao kwa ushirikiano.

"Nitafata katiba ya Chama katika kutetea maslahi ya Chama ndani ya Mkoa wa Morogoro, na katika utendaji kazi wangu sitamuonea mtu yeyote wala kukata jina lake katika uchaguzi wa ndani ya Chama na pia naagiza Kamati ya siasa ya Wilaya kama kuna mwanachama atafanya kinyume na Sheria na taratibu pizza Chama Ikimshughulikie kwa kufata Sheria na taratibu za Chama zilizopo kwa kupata ushahidi,"alisema

Alisema kazi kubwa ya Kiongozi ni kuwa na sikio sikivu hivyo watu waache makundi ndani ya mkoa wake kwani uchaguzi umekwisha sasa ni kazi ya kujenga Chama na Manispaa yao.

Aidha alisema hawawezi kuwa Chama kikubwa Duniani kama hakijakaa vizuri katika miundombinu yake ,ameagiza ifikapo Disemba mwaka huu Kata 14 kati ya kata 29 za manispaa ya Morogoro kuhakikisha zinakuwa na mipango ya kuweka miradi imara na kujenga Ofisi Nzuri za Chama .

"Sitaki kuona kata isiyona Ofisi ya CCM,nataka kata zote ziwe na Ofisi na miradi pia iwe imara,tuna kata 29 kati ya hizo kata 15 ndio zenye miradi mikubwa na Ofisi nzuri,nitapambana kwa nguvu zote kata zote ziwe na Ofisi za kupendeza kwani ndio nembo ya Chama,"alisema Mwamsiku

# Mbunge amkabidhi Kunenge madawati 390

NA MWANDISHI WETU, CHALINZE

MBUNGE wa Chalinze Ridhiwani Kikwete amemkabidhi mkuu wa mkoa wa Pwani madawati 390 yenye thamani ya shilingi.milion 30 kupunguza tatizo la uhaba wa madawati katika Halmashauri ya Chalinze.

Aidha, alisema pamoja na uhaba wa madawati katika Halmashauri ya Chalinze bado hali ya ufaulu si yakuridhisha.

Alimuomba mkuu huyo wa Mkoa kusaidia kutatua changamoto kero katika Sekta ya elimu ili kuinua kiwango cha ufaulu tofauti na hali iliyopo kwa sasa.

Richiwani alisema ataendelea kushirikiana na Serikali na wananchi kutafuta ufumbuzi wake vikwazo vya maendeleo katika Jimbo la Chalinze.

Aliomba pia alimuomba mkuu Huyo wa Mkoa kuongezewa watumishi.katika sekta ya afya ambapo kwasasa Kuna upungufu wa zaidi ya 200 kukidhi mahitaji.

Mkuu wa Mkoa Abubakar Kunenge alimpongeza Ridhiwani kwa kutoa madawati hayo huku akiahidi kushirikiana nq Mbunge huyo pamoja na watumishi wa Halmashauri hiyo kuleta mabadiliko ya kimaendeleo kwa kutatua kero za wananchi.

Scanned with CamScanner

kahawa mkoani Kagera wali-
oshiriki kikao cha uzinduzi

ili iuzwe nchini na kuingiza
kipato kwa manufaa ya kila

kilo 78,000 mwaka 2019/2020
uzalishaji wa zao hilo ulifikia

kwa tija na uchipulishaji wa
mibuni.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia), akiongea na Mbunge wa Monduli, Fredy Lowassa (kushoto), walipokutana katika kikao kilichoandaliwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kilichofanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Mbunge huyo alikuwa ni miongoni mwa wawekezaji waliohudhuria kikao hicho. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

Scanned with CamScanner

# Homa ya nguruwe bado tishio nchini

**Na Salome Kitomari**, DODOMA

SERIKALI imesema ugonjwa wa homa ya nguruwe bado ni tishio nchini na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari, ikiwamo kutoa taarifa mapema kwa kuwa hauna kinga wala tiba.

Hayo yamo kwenye hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2021/22, iliyowasilishwa na Waziri Mashimba Mashauri, na kujadiliswa na kupitishwa na Bunge mwishoni mwa wiki.

Alisema mlipuko wa Homa ya Nguruwe (African Swine Fever - ASF) uliopuka kwa vipindi mbalimbali katika mwaka 2020/2021 na kusababisha jumla ya vifo vya nguruwe 5,428 katika halmashauri 18 Tanzania Bara.

"Ugonjwa huu hauna tiba wala chanjo hivyo nitoe wito kwa halmashauri zote nchini kutoa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa na pia pale kunapotokea mlipuko kutoa taarifa mapema kwa Wizara na kupulizia dawa ya kuua virusi ili kuzuia hasara inayoweza kuwapata wafugaji," alisema.

Alisama Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kama Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) iliandaa na kuhuisha mikakati ya kuzuia magonjwa mbalimbali yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama kwa kutumia dhana ya Afya.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, mwaka 2020/2021 jumla ya ng'ombe 1,036,769, mbuzi 680,906 na kondoo 192,906 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa kimeta katika mikoa ya Arusha, Songwe, Manyara na Kilimanjaro.

Aidha, alisema jumla ya mitamba 162,843 imechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kutupa mimba katika Wilaya za Arusha, Karatu, Babati, Dodoma Jiji, Simajiro, Iringa na Njombe.

Alisema jumla ya matukio 210 ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa yalifuatiliwa na sampuli 610 zilichukuliwa ambapo mbwa 812,712 na paka 4,152 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

"Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa umeendelea kufuatiliwa kwa kukagua na kuchukuwa sampuli kwa wanyama wote wanaotupa mimba kutokana na mwaka huu kuwa na mvua nyingi," alisema.

## As

**Na Renat**

IDARA ya
isha kazi a
Uhamiaji
Salaam kw
nguvu dhi
Kyai, anay
Kamish
aji, Dk. A



Ofisa
tophe
kwan
Afya
sha u
ghara

## W

**Na Mw**

KAMI
zalish
imezi
mrad
na ku
juu y
nu sa
Uzi
2021
bapo
wata
gozi
Mku
Kalo
yefa
ya M

# Lakes yielding more fish than the ocean

By Songa wa Songa, Dodoma

LAKES Victoria and Tanganyika beat the much more expansive Indian Ocean by far in fish yield and resultant revenues, latest statistics show.

Budget speech data of the Ministry of Livestock and Fisheries indicates that the two lakes accounted for 78 per cent of fish output for the period of one year up to April 2021, while fishing along the seashore yielded 15.61 per cent of total catch.

As of April 2021, around 422,859.78 tonnes of fish worth 2.62trn/- were harvested, and out of that catch, about 234,849.99 tonnes equal to 55.54 per cent came from Lake Victoria and 96,876.02 tonnes representing 22.91 per centc came from Lake Tanganyika, the data indicated

9 770856 542009 >

Lake Nyasa accounted for 11,560.56 tonnes ( 2.73 per cent) and 13,567.33 tonnes (3.21 per cent) was harvested from smaller water bodies, on the basis of the budget estimates tabled by the Livestock and Fisheries minister, Mashimba Ndaki.

In the next financial year the government will focus on the blue economy, delivering heavy investments aimed at reaping the benefits of the sea expanse in the country's territorial waters and exclusive economic zone, he said.

The state is out to invest heavily in deep sea fishing so as to improve productivity in the sector, he said, noting that the government is going to purchase four modern deep sea fishing vessels; with two expected to be based in Zanzibar and two on the Mainland-.

In the outgoing financial year up to 195,435 people were engaged in fishing as an economic activity with using about 58,231 vessels of various types, he said, showing that the contribution of the sector to the Gross Domestic Product was a meager 1.71 in 2020, even as it grew at the rate of 6.7 per cent.

The parliamentary committee for Agriculture, Livestock and Water blamed the government for failing to disburse

TURN TO PAGE 2

Sa
of

By Gu

PRI
has r
the li
secre
offici
Com
Comp
Acc
Com
Msig
Willi
Natio
to h
Mdu
Fo
Gen
Mpo
Regi
Com
head
Ba
min
Japa
RAS
N
Dire
RAS
DEI
tran
P
Mu

Residents of Matepwende village in Namtumbo District in Ruvuma region sort sesame at the weekend ... Warehouse Receipt system. Photo: Guardian Correspondent

# Adding value to livestock diversity will increase productivity, MPs say

Songa wa Songa, Dodoma

LOW productivity in livestock sector that caused a heated debate in in the National Assembly here last week is linked to slow pace in value addition, statistics show.

Data in the Ministry of Livestock and Fisheries 2021/22 budget estimates show that out of the 3 billion litres of milk produced in that financial year, only 75.9 million were processed.

Also, the numbers show that there is a snail's pace in embracing modern breeds of dairy cows, hence low milk production from the over 30 million cattle in the country.

"Some 2.17 billion litres of milk came from traditional cattle while 93 million were from modern breeds," reads the speech read by Livestock and Fisheries Minister Mashimba Ndaki.

Out of the 33.9 cattle currently in the country, only 1.2 million are dairy cows, the Minister said.

"In the financial year 2020/21, milk processing stood at 30 per cent of installed capacity," Ndaki said.

"By 30 April 2021, there were a total of 99 milk processing plants out of which 96 were operating while three were not working at all due to a number of challenges including failure to endure business competition."

The minister added that as of 30 April 2021; a total of 11.77 million pieces of animal skins worth 25.93bn/- were produced but only 1.50 million pieces worth 16.1bn/- were exported.

As for leather quality, the minister said that a lot needs to be done to education cattle keepers in the country on how to take care of animal skins because billions of shillings are lost annually due to poor quality of animal skins.

"A lot of skins are full of marks ranging from identification to slashing; this compromises the quality of our skins in the international market," he said.

Ndaki said that the number of all types of livestock in the country went up in 2020/2021 compared to 2019/2020 with cattle increasing from 33.4 million to 33.9 million; goats went up to 24.5 million from 21.29 million and sheep increased from 5.65 million 8.5 million.

Also, the number of chicken has gone up from 83.28 million to 87.7 million and pigs from 2.14 million to 3.2 million.

But as for productivity, the statistics painted a grim picture with the sector growing at a meager 5 per cent in 2020 and *contributing only 7.1 per cent* to the Gross Domestic Product, down from the 7.4 contribution to the GDP in 2019.

ACHIEVE

er

laus
its
cial
and
the

ion
lish
ant
its

cus
ith
ills
to
ll-
ty

ed
in
te
p
n,
es
s

y



**Livestock and Fisheries minister Mashimba Ndaki (R) has a quick word with Monduli legislator Fredy Lowassa on the sidelines of a meeting organised in Dodoma city at the weekend by the National Ranching Company.** Photo: Guardian Correspondent

Scanned with CamScanner

Mwananchi umebaini wapi-gapicha hao hujiingizia kati ya

ujenzi wa nyumba ya vyumba viwili na sebule ninayoishi na

# Kiwanda cha maziwa Baraki chapigwa jeki

Beldina Nyakeke, Mwananchi

Rorya. Ili kuongeza uzalishaji, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini ( IRDP) kitakipatia kituo cha Baraki Sisters kilichopo wilayani Rorya mashine maalum ya kuchemsha na kupooza maziwa kuharakisha uongezaji thamani.

Ahadi hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na mkuu wa chuo hicho, Profesa Hozen Mayaya alipotembelea kituo hicho kinachotoa huduma za kijamii huku kikiwajenga wananchi kiimani.

Mashine hiyo yenye uwezo wa kuchemsha na kupooza lita 300 za maziwa kwa saa moja, itasaidia kuongeza fursa za kiuchumi na soko la maziwa kwa wakazi wa Kijiji cha Baraki na halmashauri kwa ujumla.

Mwakilishi mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa ( UNDP), Christine Musisi aliahidi kumtafuta mfadhili atakayesaidia upanuzi wa usindikaji maziwa kusaidia kuboresha lishe ya watoto na kuongeza kipato cha wafugaji wanaokosa solo la uhakika.

Mkuu wa Wilaya ya Rorya, Simon Odunga alisema Serikali inatekeleza mikakati ya kufufua kiwanda cha maziwa Utegi kitakachokuwa na uwezo wa kuchakata lita 4,000 za maziwa kwa siku hivyo kusaidia kuongeza tija wilayani Rorya.

Mkuu wa kituo cha Baraki, Sister Jenipha Mabonyesho alisema kwa sasa, wana uwezo wa kuhifadhi lita 2,100 za maziwa kwa siku hali inayowalazimisha wafugaji kusafiri zaidi ya umbali wa kilomita 80 kwenda Tarime Mjini au Musoma kupeleka maziwa.

Tanzania inazalisha zaidi ya lita bilioni 2.3 za maziwa lakini kiasi kidogo tu ndicho husindikwa.